Huduma ya Hana
TWR

**Juni 2016**

Mpendwa mshirika katika maombi,

Nimetiwa moyo mkuu sana wiki hii kujua kuwa tunapokatishwa tamaa, mioyo yetu inaweza kupata pumziko kwa Mungu tunapoyapata matumaini kupitia kwake (Zaburi 62:5).

Tunaweza kumkabidhi hofu zetu zote na kutiwa moyo kutokana na ukweli kuwa hakuna lisilowezekana kwa Mungu (Luka 1:37). Tunapokuja pamoja kuomba, sauti zetu zinaufikia moyo wa Mungu na tunapokea ujasiri wa kukabiliana na matatizo yetu, upinzani na magumu yote.

Kwa maombi, maisha yetu yanaguswa na kuponywa.Hizi hapa ni baadhi ya shuhuda kutoa Msumbiji:

*"Nilipoanza kuomba, nilifikiri sitafikia mwisho, lakini Mungu alikuwa pamoja na mimi. Maombi yangu nikuiona familia yangu ikiwa na amani. Nilipokuwa naendelea na maombi, binti yangu akaja nyumbani na kumuomba baba yake msamaha kutokana na jambo lililowatenganisha. Kwa namna hii, nikaiona nguvu ya maombi."*

*Hakuna mwenye nguvu za Mungu ila tunapoomba, Mungu anaweza kufanya kazi yake ya miujiza kupitia maombi yetu."*

Tunapokusanyika ulimwenguni kuwaombea dada zetu wa Angola na Msumbiji, tukumbuke jinsi 1 Samueli 1,Mungu aliyasikia maombi ya Hannah.Alikuwa amekata tamaa,ameudhika na mwenye uhitaji mkubwa wa mtoto. "Katika uchungu wake Hannah akamuomba MUNGU, akilia sana" (1 Samueli 1:10).

Tukumbuke kuwa hata tuchukie na kukatishwa tamaa kwa kiwango gani, Mungu yupo karibu na anasikia maombi yetu. Kuomba kila siku pamoja na maelfu ya wanawake ulimwenguni hutuletea umoja na nguvu iliyopo ndani ya mwili wa Kristo.

Asante kwa kujitoa na kutenga muda wa kuinua sauti yako katika maombi. Uamini leo kuwa Mungu anasikia maombi yako na takujibu kwa njia yake iliyo bora kwa kwa wakati unaofaa.

*"Huu ndio ujasiri tulionao wa kumuendea Mungu: kwamba tukimuomba kitu kulingana na uhitaji wake, anatusikia – lolote tuliombalo – tunajua kuwa tunacho kile tulichokiomba" (1 Yohana 5:14).*

Katika yeye, mioyo yetu inashangilia,

Peggy Banks
Mkurugenzi wa Huduma wa Kimataifa
Project Hannah

**Shuhuda za Msumbiji:**

Unapomuamini Mungu, atakutumia uwe mikono yake. Ndoa yangu ilikuwa mgogoro, lakini nikaanza kumuomba Mungu auteke moyo wa mume wangu. Najua ilinichukua muda mrefu kwa Bwana kuumiliki moyo wa mume wangu na kuulanisha moyo wangu kwanza. Ushauri wangu kwa dada zangu ni kwamba tunapokuwa na matatizo tuwe wavumilivu na Mungu atatupa jibu zuri.

Nitaelezea kinachoendelea kwenye maisha yangu dada zangu. Mimi ni mtoto wa tatu kuzaliwa kwa wazazi wangu. Nilipovunja ungo, baba yangu alinifanya niolewe na mtu aliyekuwa mganga wake. Nilikuwa mke wa nne na nikaambiwa hakuna kwenda kanisani. Nina watoto watano kwenye ndoa hii, na nilitamani kuwaona wakiondoka kwenye mateso haya. Kuna wakati nilikuwa naomba kwa siri maana mume wangu alikuwa akinikuta naomba, ananipiga. Halafu siku moja, mtoto wangu wa kwanza akawa na rafiki aliyempeleka kanisani. Huyo rafiki alikuja nyumbani kwetu na kumuomba mume wangu amruhusu kijana wangu awe sehemu ya huduma ya vijana kanisani kwao. Kwa siku mbili nililia kwa hofu kwamba kijana wangu ataadhibiwa. Lakini mume wangu akaniomba kama mama wa mtoto niwe naenda naye kila jumapili ili nidhibiti nyendo zake. Nikafikiri kuwa si kweli kwamba hili lilikuwa linafanyika, kwamba Mungu alikuwa ananiruhusu mimi na kijana wangu kufanya kile nilichokitamani kwa muda mrefu sana. Mungu anaishi. Sasa naweza kusema mimi ni mkristo, na nimejiunga na huduma ya Project Hannah. Omba pamoja na mimi ili siku moja niione familia yangu ikiwa kanisani.

Nilipoolewa, sikujua mwanzoni kuwa mume huyu alikuwa anatumia madawa ya kulevya. Alikuwa anajifanya kuishi kama mkristo. Baada ya muda, akaanza kuniumiza – hadi tukatengana. Nikawa mwanamke anayeteseka. Kisha nikakisikia kipindi cha Wanawake wa Matumaini kwenye redio. Baada ya mwaka mmoja ya kuvisikiliza vipindi hvi, nikaanza kuwapigia simu waandaaji ili niweze kuwa sehemu ya familia hii. Mwaka jana nikaanza kukutana na wanawake wengine waliokuwa wanamkabidhi Mungu shida na matatizo yao. Ilikuwa vigumu sana kuwashirikisha shida zangu, lakini siku moja nikajiona nakaukiwa kutokana na umaskini uliokuwepo nyumbani kwangu. Nina mtoto mmoja. Hivi sasa mimi ni mtu mpya. Nina matumaini kuwa mizigo yangu yote niliyomuachia Mungu itakuwa miepesi. Sasa hivi nafanya kazi, ya huduma za nyumbani na pia namtunza mwanangu mzuri mdogo. Mungu anayajua maisha yangu na analo kusudi kwa ajili yangu.

**Shuhuda za Angola:**

Mwanamke aliyenyanyaswa kwa miaka 15 na kudhihakiwa kuwa ni tasa alijiunga na kikundi cha maombi cha Project Hannah mwaka 2013. Kwa kuvisikiliza vipindi,kufunga,kuomba na kushirikisha, Mungu akajibu maombi yake na kumponya. Sasa ameshabeba mimba na ana mtoto wa miezi miwili.

Asante Mungu! Niliwashirikisha watu wa kikundi cha maombi cha kanisani mwangu kuhusu ugonjwa uliomuandama mwanangu kwa muda wa miezi saba. Alikuwa anatapika kila alipokula au kunywa. Kwa neema na rehema ya Mungu amepona na amempokea Yesu.

Mratibu wa Project Hannah Angola alitembelea kituo cha El Bethel Center, kinachowahifadhi vijana 50 na watoto wa mtaani wachache. Mwezi uliofuatia, wanawake wa Project Hannah wakatembelea kituo hicho cha El Bethel Center na kuwapelekea vitu vya matumizi yao na kufanya nao kikao.